



## **TAARIFA KWA UMMA /VYOMBO VYA HABARI**

### **UBINAFSISHAJI WA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na mchakato wa kuibinafsisha Benki ya Watu wa Zanzibar(PBZ) na inakusudia kuuza asilimia sitini (60%) ya hisa zake kwa muwekezaji kupitia mchakato wa mnada-umma (public bidding process).

PBZ ni benki inayoongoza kwa Zanzibar na mwezi Desemba 2005 ilikuwa na amana zenyé thamani ya Shilingi 60.5 bilioni.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawakaribisha wawekezaji watakaoongeza mtaji, wenyé uwezo na uzoefu na wakiwa na ari na sera za ubunifu kwa ajili ya kuendesha benki. Ubinafsishaji wa benki unategemewa kuleta mageuzi na mabadiliko ya uchumi wa Zanzibar kutoka kuwa uchumi wa msingi wa kutumia sana fedha cash based economy na kuwa uchumi wa msingi wa kutumia huduma za kibenki bank based economy na hivyo kuwezesha utoaji wa huduma za kibenki za kisasa zaidi. Huduma za kibenki sio tu zitaimarishwa kwa kutumia vifaa vya kisasa, bali pia

zitakuwa nyingi na nzuri zaidi, hususan utoaji mikopo utahuishwa ili kuwezesha utoaji mikopo midogomidogo na ya kati kwa umma.

Ili kuhakikisha kuwa malengo haya yanatimia, waombaji watarajiwa watapitia mchakato wa awali wa kuchujwa ambapo yule aliye bora atachaguliwa kwa kuzingatia uwezo wake wa kifedha uzoefu na malengo ya Serikali ya kubin afsishwa benki. Inategemewa kuwa atakayeshinda (preferred bidder) mnada-umma atachaguliwa mwezi Machi 2007 kutoka orodha ya wawekezaji walioomba.

Katibu Mkuu,  
Wizara ya Fedha na Uchumi,  
Serikaliya Mapinduzi Zanzibar  
S. L. P 1154  
**Zanzibar**